

**TAARIFA KWA UMMA****TANGAZO LA NAULI ZA ABIRIA KWA DARAJA LA KAWAIDA -  
TRENI YA RELI YA KISASA (SGR), 2024**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawatangazia taarifa ya maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kuhusu nauli za abiria wa daraja la kawaida kwa Treni ya Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora. Nauli hizi ni baada ya kufanya kazi maombi yaliyoletwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na taarifa zilizopokelewa kutoka TRC na wadau wengine.

Kuelekea kuanza kwa safari za SGR Dar es Salaam mpaka Makutupora, masharti ya kuzingatia kabla ya kuanza kutumika kwa nauli hizi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mto huduma (TRC) kuwa na lesseni ya usafirishaji;
- (ii) Kuwa na ithibati ya usalama wa miundombinu ya reli na mabehewa;
- (iii) Kutumia mfumo wa utoaji wa tiketi za kielektroniki;
- (iv) Kuunganisha mfumo wa tiketi za kieletroniki na mifumo ya LATRA;
- (v) Kukokotoa malipo na utunzaji taarifa za abiria, nauli iliyolipwa, tiketi za kielektroniki zilizotolewa, kodi za Serikali na tozo za kisheria; na,
- (vi) Kuwa na watumishi wa kada muhimu kwa masuala ya ufundi na uendeshaji wa treni ya SGR ikiwa ni pamoja na madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA.

Aidha, nauli hizi ni kwa daraja la kawaida kwa watu wazima na watoto kuanzia umri wa miaka 4 hadi 12 ambapo nauli zitalipwa na abiria kwa kilomita. Nauli itakayolipwa na mtu mzima na mtoto mwenye umri zaidi ya miaka 12 ni TSH. 69.51 kwa kilomita, na mtoto kuanzia kuanzia miaka 4 hadi 12 atalipia TSH 34.76 kwa kilomita. Aidha mtoto mwenye umri chini ya miaka minne (4) hatalipa nauli, hata hivyo, taarifa zao na wasafiri wote zitatunzwa kwenye mfumo wa taarifa za abiria wanaosafiri kila siku.

Mchanganuo wa nauli hizo kwa daraja la kawaida kulingana na umbali wa vituo kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora kwa watoto wazima na watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 ni kama ifuatavyo;

Safari		Umbali (Km)	Nauli (Shilingi)
Kutoka	Kwenda		Daraja la Kawaida
Dar es Salaam	Pugu	19.0	1,000
Dar es Salaam	Soga	51.0	4,000
Dar es Salaam	Ruvu	73.0	5,000
Dar es Salaam	Ngerengere	134.5	9,000
Dar es Salaam	Morogoro	192.0	13,000
Dar es Salaam	Mkata	229.0	16,000
Dar es Salaam	Kilosa	265.0	18,000
Dar es Salaam	Kidete	312.0	22,000
Dar es Salaam	Gulwe	354.7	25,000
Dar es Salaam	Igandu	387.5	27,000
Dar es Salaam	Dodoma	444.0	31,000
Dar es Salaam	Bahi	501.6	35,000
Dar es Salaam	Makutupora	531.0	37,000

Aidha, mchanganuo wa nauli kwa daraja la kawaida kulingana na umbali wa vituo kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora kwa watoto wenye umri kuanzia miaka minne (4) hadi 12 ni kama ifuatavyo;

Safari		Umbali (Km)	Nauli (Shilingi)
Kutoka	Kwenda		Daraja la Kawaida
Dar es Salaam	Pugu	19.0	500
Dar es Salaam	Soga	51.0	2,000
Dar es Salaam	Ruvu	73.0	2,500
Dar es Salaam	Ngerengere	134.5	4,500
Dar es Salaam	Morogoro	192.0	6,500
Dar es Salaam	Mkata	229.0	8,000
Dar es Salaam	Kilosa	265.0	9,000
Dar es Salaam	Kidete	312.0	11,000
Dar es Salaam	Gulwe	354.7	12,500
Dar es Salaam	Igandu	387.5	13,500
Dar es Salaam	Dodoma	444.0	15,500
Dar es Salaam	Bahi	501.6	17,500
Dar es Salaam	Makutupora	531.0	18,500

Vile vile Maeneo ya msingi ya kuzingatiwa na Mtoa Huduma ni pamoja na;

- Kuweka mfumo wa usimamizi wa utoaji taarifa kwa wasafiri (Passenger Management Information System) na mfumo wa ufuatilaji wa mwenendo wa treni (Train Tracking System);
- Kuweka nauli za safari ya kituo kwa kituo katika maeneo yanayoonekana na abiria kiurahisi kwa wakati wote;
- Kuhakikisha uwepo wa huduma bora kwa wateja ikiwemo mazingira ya vituo (stesheni), usafi wa mabehewa, chakula na vinywaji, maji safi na salama, mwanga wa kutosha, na kuweka utaratibu wa fidia dhidi ya majanga na upotevu wa mizigo ya abiria; na
- Kuzingatia vigezo vya usalama wa mabehewa na miundombinu ya reli kwa mujibu wa Sheria, Kanuni za Taratibu zilizopo.

Salum Pazzi  
**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**